Kujifunza Jinsi Ya Kufanya Kazi Na Watoto Yatima Na Wale Waishio Katika Mazingira Hatarishi Zaidi.

Mradi wa Ustawi wa Jamii kuhusu VVU/UKIMWI unaoendeshwa kwa ushirikiano kwa ajili ya watoto yatima na wale waishio katika mazingira Hatarishi zaidi Tanzania.

Siku ya 8

Ufuatiliaji na Tathimini , Kushughulikia Unyanyapaa na Ubaguzi

Malengo

Kufikia mwisho wa siku Msaidizi Ustawi wa jamii ataweza ku:

- Kuelezea dhana ya msingi na mchakato wa ufuatiliaji na Tathimini wa shughuli za watoto waishio katika mazingira hatarishi zaidi katika ngazi ya kijiji na kata.
- Onyesha uwezo wa kutumia fomu za kuandikia taarifa za watoto waishio katika mazingira hatarishi zaidi.
- Tambua mambo yanayochangia unyanyapaa kuhusu VVU na / au kuwa mtoto aliye katika mazingira hatarishi
- Tambua madhara ya unyanyapaa na ubaguzi
- Tmbua hatua zinazo weza kuchukuliwa katika ngazi ya jamii ili kupunguza unyanyapaa.

Ufuatiliaji Na Tathimini

Ufuatiliaji Na Tathimini

- Nini maana ya ufuatiliaji?
- Nini maana ya Tathimini?
- Ni mifano gani ya ufuatiliaji na Tathimini uliyowahi kufanyaia kazi?

Bungua Bongo katika vikundi vidogo na mjadili

Ufuatiliaji Na Tathimini

Nini maana ya ufuatiliaji?

Ufuatiliaji *unahusisha ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa ili kutambua jinsi shughuli* zetu zinavyoendelea ukilinganisha na malengo tuliyojipangia.

Nani hufanya ufuatiliaji?

- Ufuatiliaji hufanywa na wadau mbalimbali wa programu au mradi.
- Kwa mfano, ufuatiliaji katika programu ya PSW hufanywa na:
  - Wasaidizi Ustawi waJamii
  - Wasimamizi
  - Maafisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya
  - Shirika la Intrahealth
  - Chuo cha Ustawi wa Jamii na wadau wengine wa Maendeleo.

Nini maana ya Tathimini?

- Tathimini ni mchakato wa kupima wenye malengo ya kuangalia utaratibu, utekelezaji, maboresho au matokeo ya programu.

Source: Rossi, P.H,& Freeman, H.E (1993). *Evaluation: A systematic approach* (5th ed.). Newbury Park, CA:Sage Publications, Inc

Je Tathimini Hufanya Nini?

- Kama ilivyo kwenye ufuatiliaji, Tathmini hufanywa na wadau mbalimbali katika mradi na programu:
- Mfano ufuatiliaji katika programu ya PSW hufanywa na:
  - Wasaidizi Ustawi waJamii
  - Wasimamizi
  - Maafisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya
  - Shirika la Intrahealth
  - Chuo cha Ustawi wa Jamii na wadau wengine wa Maendeleo

Uhusiano Uliopo Kati Ya Malengo Ya Programu Na Tathimini

Nini Maana Ya Lengo?

- Lengo ni kile ambacho msaidizi ustawi anacho dhamiria kukifikia kwa kutoa huduma kwa watoto na familia zaondani yamuda aliojipangia
- Je unaweza kufikiria baadhi ya malengo ya ujumla kuhusu yale unayodhamiria kuyafikia katika kuwa saidia watoto na famialia?

Kwanini Tuweke Malengo?

- Malengo huongoza shughuli tulizojipangia kuzifanya ili kufikia matoleo tunayoyatarajia
- Huhamasisha uwajibikaji– Husaidia kuthibitisha kuwa kweli tunatekeleza yale tuliyo kusudia
- Malengo hutuwezesha kufafanua jukumu la kila mtendaji katika tutatua tatizo.
- Kuainisha matokeo ya programu:
  - Malengo hutuwezesha kujifunza kuwa kama tume tatua tatizo au la.

Nini Maana Ya Malengo?

- Malengo mahususi ni kusudi maalumu linalolenga kufikia lengo kuu. Ambalo lina weza kuwa ni idadi kadhaa ya matokeo mengine.
- Je unaweza jufikiria mfano wa lengo linalowezesha kufikia lengo kuu ulilokusudia hapo awali?

Malengo

- Mfano wa lengo linalowezesha kufikia lengo kuu ulilojiwekea
- Lengo la ujumla kwa kawaida ni la muda mrefu kama vile kupunguza idadi ya watoto waishio katika mazingira hatarishi katika wilaya ya Chamwino kwa 20% ifikapo 2012
- Lengo mahususi linaweza kuwa kuboresha kumbukumbu kuhusu jinsi kiasi cha huduma unazotoa kwa watoto waishio katika mazingira hatarishi zaidi ifikapo Desemba 2012

Nani Anapaswa Kuweka Lengo Na Malengo?

- Wadau wa programu katika ngazi zote.
- Wasaidizi Usawi wa jamii.
- Wasimamizi
- Maafisa Usawi wa Jamii wa Wilaya.
- Shirika la Intrahealth,Chuo cha Ustawi wa Jamii.

Mambo Gani Ya Kuzingatia Unapoweka Malengo?

- Muda wa programu/mradi
- Malengo yaweze kufikika na kupimika
- Chagua viashiria muhimu vinavyoonyesha ushahidi(tarakimu inayoweza kuhesabu rasilimali au matokeo)
- Vitendea kazi au vifaa vitakavyosaidia kufanya kazi (baisikeli, vifaa vya kuandikia)
- Hali ya hewa na mazingira kwa ujumla vinavyoweza kuathiri matokeo (mafuriko, msimu wa joto,mvua,kukosekana kwa rasilimali kuugua n.k.)
- Ni kitu gani kimekwenda vizuri(mafanikio uliyowahi kuyafikia) na vipi ni vikwazo au changamoto vinavyoweza kuzuia kufikia malengo yetu

Katika Kuweka Malengo Ya Mradi Wa Wasaidizi Ustawi Wa Jamii: Kumbuka…

- Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inapendekeza kuwa kila mtu anayejitolea anapaswa ahudumie ***sio zaida ya watoto 20 kila mwezi.***

Tathimini Ya Huduma Kwa Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi Zaidi Na Familia Zao.

Tathimini Ya Huduma Kwa Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi Zaidi Na Familia Zao

- Tutapitia dondoo zilizo kwenye dodoso la Hali ya Mtoto (CSI).
- Tujaribu kufikiria malengo tunayoweza kuyapima.
- Unafanyakazi na watu wengine wa 2-3 kwa dakika 5 kisha tutapeana mrejesho toka kwa kila kikundi.

Ufafanuzi Wa Huduma Kwa Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi Zaidi

- Chakula na Lishe-Huduma kwa watoto au watu wengine ndani ya kaya ili kuwawezesha kuwa na chakula cha kutosha na chenye muendelezo wa upatikanaji ili kukidhi mahitaji yao ya lishe.

Ufafanuzi Wa Huduma Kwa Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi Zaidi

- ***Makazi:*** Huduma inayo wezesha mtoto kuwa na mahali salama pa kuishi, panapofaa na pakavu kulingana na kanuni za jamii husika.
- Mtoto pia anaweza kupata huduma ya maji safi ya kunywa, anaishi katika mazingira safi na anayo mavazi.

Ufafanuzi Wa Huduma Kwa Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi Zaidi

- ***Ulinzi:*** Huduma inayo hakikisha kuwa mtoto yuko huru dhidi ya unyanyasaji,kutojaliwa,na aina zote za utumikishwaji na anao ulinzi wa kisheria wa kutosha.

Ufafanuzi Wa Huduma Kwa Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi

- ***Afya:*** Huduma inayo hakikisha kuwa mtoto na watu wengine ndani ya kaya wanaweza kuzifikia huduma za Afya ya msingi ambazo zinajumuisha kinga na tiba pamoja na elimu ya afya chanjo,VVU/UKIMWI, Unasihi na Tathimini na Huduma ya maji taka.

Ufafanuzi Wa Huduma Kwa Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi

- ***Msaada wa Kisaikolojia:*** Huduma inayohakikisha kuwa mtoto anafurahia uhusiano mzuri na watu wazima pamoja na watoto wengine, anahisi utoshelevu na ni mwenye kujiamini.

Ufafanuzi Wa HudumaKwatoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi Zaidi

- ***Elimu na Mafunzo:*** Huduma inayohakikisha kuwa mtoto ameandikishwa , anahudhuria, na nafanya vizuri shuleni /mafunzo ya ufundi stadi au kazi inayolingana na umri.
- Watoto walio chini ya umri wa kwenda shule wanahamasishwa kwa michezo,simulizi za hadithi, kuimba, na kushiriki katika shughuli za kijamii.

Ufafanuzi Wa Huduma Kwa Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi

- Kuimarisha Uchumi wa familia: Huduma inayo wawezesha wazazi au wakuu wa kaya kuweza kukidhi huduma za msingi kwa watoto waishio katka mazingira hatarishi zaidi bila kutegemea msaada toka nje.

Mrejesho: Tathimini Wa Huduma Zetu

- Jadili.

Kwa Nini Tunahitaji Takwimu Katika Ufuatiliaji Na Tathimini

Majadiliano Katika Kundi Kubwa Kuhusu Umuhimu Wa Takwimu

Jadili:

- Kwanini tukusanye takwimu?
- Nani anahitaji tawimu tunazokusanya?
- Ni maamuzi ya aina gani yanayofanywa yanayotolana na matokeo ya takwimu zetu?

Kwanini Tunakusanya Takwimu?

Tunakusanya takwimu zitusaidie:

- Kupima mafanikio yetu na changamoto
- Kupanga mipango ya maendeleo ya kazi katika vijiji, kata na wilaya.

Nani Anahitaji Takwimu Zetu?

- ***Takwimu zetu zinahitajiwa na watu mbalimbali:***
- Serikali(Vijiji, Kata, Mkoa na Taifa
- Mashirika yasiyo ya kiserikali(NGOs)/vyama vya kijamii
- Watu binafsi
- Wafadhili kama benki ya Dunia, USAID,n.k.
- Sisi wenyewe!

Ni Maamuzi Ya Aina Gani Yanayofanywa Kutolana Na Matoleo Ya Takwimu Zetu

- Kufanya maamuzi kuhusu mgawanyo wa rasilimali. Kama vile rasilimali gani zielekezwe wapi?

Mfano: Ni watoto wangapi waishio katika mazingira hatarishi zaidi wanahitaji aina gani ya huduma?

- Tengeneza mikakati ya kushughulikia changamoto mbalimbali za maendeleo
- ***Mfano:*** Jinsi ya kusaidia familia za watoto waishio katika mazingira hatarishi zaidi kupata huduma za kuimarishwa kiuchumi

Rejea Fomu Ya Ufuatiliaji Na Tathimini

Fomu Ya Tathimini



Mfumo Wa Utoaji Taarifa Wa Wasaidizi Ustawi Wa Jamii



Unyanyapaa Na Ubaguzi

Utangulizi

- Watoto yatima na wale waishio katika mazingira hatarishi hunyanyapaliwa kwasababu ya:
  - VVU/UKIMWI
  - Hali ya familia

Nini Maana Ya Unyanyapaa?

Jadili na Bangua Bongo

Maana Ya Unyanyapaa

- Unyanyapaa ni hali ya kutokukubalika kwa sifa za mtu kijamii, kimazingira au kiimani ambazo ni kinyume na kanuni za mila na desturi ya jamii husika.
- Ni nyenzo imara ya kuitawala jamii
- Hutumika kukandamiza, kubagua, kuonyesha uwezo dhidi ya watu wenye sifa fulani

Kwanini watu hunyanyapaliwa? Je tunaweza kufanya nini kuhusu unyanyapaa?

Bungua Bongo

Kwanini Watu Hunyanyapaliwa?

- Imani za kimila
- Hofu
- Mfumo wa imani nje ya ufahamu wenye mantiki.
- Kukosa Elimu.

Mambo Yanayochangia Unyanyapaa Kuhusu VVU/UKIMWI

- VVU/UKIMWI ni ugonjwa unaotishia maisha.
- Watu wanayo hofu ya kuambukizwa VVU.
- VVU vina uhusiano na tabia ambazo tayari zinanyanyapaliwa.
- Watu wenye VVU/UKIMWI wanadhaniwa kuwa wanawajibika kwa kupata maambukizi.
- VVU/UKIMWI mara nyingi huonekana kuwa ni matokeo ya mmomonyoko wa maadili unaostahili adhabu.

Sura Inayoimarisha Unyanyapaa

- VVU/UKIMWI kama adhabu
- VVU/UKIMWI kama Jinai
- VVU/UKIMWI kama Vita
- VVU/UKIMWI kama kitisho
- VVU/UKIMWI kama mengineyo

Aina Za Unyanyapaa Unaohusiana Na VVU/UKIMWI

- Sheria,kanuni na sera.
- Muitikio wa ngazi ya jamii.
- Wanawake
- Familia
- Ajira
- Huduma za Afya
- Ukanaji.

Ni Kwa Jinsi Gani Unyanyapaa Huwa Ni Kikwazo Katika Upatikanaji Wa Huduma Za VVU?

- Unyanyapaa – kwa mtubinafsi
  - Unafikia kiwango cha kukubali tiba ila hutaki kuwa wazi kuhusu hali yako kwa wanafamilia na jamii ambao wangeweza kuwa wa msaada katika kukufanya uzingatie matibabu na dawa.
- Unyanyapaa- unaoletwa na familia na jamii
  - Watu ndani ya familia na/au jamii hukuzuia kuzingatia Tiba dhidi ya VVU kwa kukukandamiza vurugu au kukutenga.

Ni Zipi Athari Za Unyanyapaa Unaohusiana Na VVU?

- Kwa watu wazima
- Kwa watoto

Bungua Bongo

Ni Zipi Athari Za Unyanyapaa Wa VVU Kwa Watu Wazima?

- Watu kutopima VVU
- Ikiwa hawajapima, watu hawachukui tahadhari ya kuzuia maambukizi ya VVU huvyo huendelea kuambukiza pasipo kujua.
- Watu hawapati matibabu, wanajiweka wao wenyewe , wenza wao na wanafamilia katika hatari ya kifo kisicho cha lazima.
- Watu wanaofahamu hali zao kuhusu maambukizi ya VVU hawawaelezi wana familia hivyo huwa wasambazaji wa ugonjwa
- Wanawake wajawazito ambao hawako tayari kupima afya zao wanauwezekano mkubwa wa kuwaambukiza watoto wao.
- Familia huachwa na wajane , yatima, na mzigo mkubwa wa matatizo ya kijamii, kiuchumi, na kihisia.
- Umasikini huongezeka

Ni Yapi Madhara Ya Unyanyapaa Kwa Mtoto?

- ***Watoto hutengwa na familia na msaada.***
  - Watoto wanao nyanyapaliwa wanaweza kujeruhiwa, kuuwawa au hata kutelekezwa.
  - Watoto wanaweza kunyimwa huduma kama vile shule,huduma za afya au kupata mahitaji ya msingi
  - Watoto wanaoweza kuhimili wanakuwa na hisia za kutokuwa na thamani

Ni Yapi Madhara Ya Unyanyapaa Kwa Mtoto?

Hali kama hizi huchangia kuwepo kwa matatizo ya ziada ikiwemo:

- Watoto huweza kudhuriwa na/au kuuwawa
- Watoto wanaweza kudharauliwa au kudhihakiwa
- Imani kuhusu hali ya mtoto au mzazi kuhusu VVU huweza kutumika vibaya kumdhibiti mtoto.
- Mambo yote haya huambatana na makuzi ya mtoto
- Jamii hukosa uzalishaji unaochangiwa na watoto na vijana.
- Familia zinaachwa na wajane,yatima na upungufu mkubwa kijamii, kiuchumi na mzigo wa hisia.
- Umasikini huongezeka
- Kukosekana kwa uimara wa kijamii.

Je Tunawezaje Kubadili Jumbe Hizi Ili Kupunguza Unyanyapaa Kuhusu UKIMWI?

- VVU/UKIMWI ni hukumu ya kifo
- Watu wanayo hofu ya kuambukizwa VVU kwa njia ya kawaida.
- VVU vinahusishwa na tabia ambazo tayari zinanyanyapaliwa.
- Watu wenye VVU/UKIMWI wanawajibika kwa kupata na maambukizi
- VVU/UKIMWI mara zote huonekana kama adhabu kwa dhambi zinazostahili.

Je Tunawezaje Kusaidia?

- ***Katika ngazi ya jamii***
  - Sheria
  - Elimu
  - Ufuatiliaji
  - Mazingira yanayowezesha
  - Ujumbe kwa jamii

Je Tunawezaje Kusaidia?

- ***Ngazi ya mtu binafsi***
  - Hamisha mtazamo wa mtoto toka hisia za kutokuwa na thamani kuelekea kuwa mwenye uwezo na matumaini.
  - Ukabili ukandamizaji na kutokujumuishwa kwa kuwahakikishia watoto kuwa wamejumuishwa kwa kuwa na mahusiano binafsi pamoja na mazingira kwa upana wake.

Je Tunawezaje Kusaidia?

- ***Fanya kazi kuhakikisha kuwa mtoto amejumuishwa kwenye:***
- Taarifa
- Watu muhimu
- Njia ya msaada
- Uwanachama wa kikundi
- Majukumu yenye maana
- Vyanzo vya furaha
- Uthamani na maadili
- Historia yake binafsi
- Sehemu